



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA  
BIASHARA

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA



ISO 9001:2015 Certified

Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali

## UFAFANUZI KUHUSIANA NA TAMBI ZENYE CHAPA YA SANTA LUCIA

Dar es Salaam, 11 Aprili, 2023

Hivi karibuni, kumekuwepo na taarifa inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii inayoonesha bidhaa ya tamba yenye chapa ya *Santa Lucia* iliyoandikwa maneno “for sale in Tanzania only” ikiwa na maana “Ni kwa ajili ya kuuzwa Tanzania pekee” katika kifungashio chake.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kufafanua kuwa bidhaa hiyo inazalishwa na kiwanda cha Tanzania Pasta Industries Limited kilichopo Vingunguti eneo la viwanda, jijini Dar es Salaam na imethibitishwa ubora wake kupitia Leseni Na. 2125 baada ya kukidhi matakwa ya Kiwango cha Kitaifa cha tamba (TZS 615: 2022, *Pasta products — Specification*).

Aidha, Kiwanda cha Tanzania Pasta Industries Limited kimekubaliana kibiashara na mmiliki wa chapa ya *Santa Lucia* kuzalisha bidhaa hiyo kwa mujibu wa Sheria za Tanzania na kuuza nchini Tanzania pekee ambapo makubaliano hayo ndiyo yaliyopelekea kuandikwa maneno ya “for sale in Tanzania only” kwenye kifungashio kwa ajili ya kudhibiti masoko.

Hivyo basi, uwepo wa maneno “for sale in Tanzania only” hauna uhusiano na masuala ya ubora au usalama wa bidhaa hiyo kama taarifa hiyo inavyodai bali ni kwa minajili ya mipaka ya kibiashara baina yao (*Franchise boundary*).

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **0800110827**

Gladness H Kaseka  
Meneja wa Uhusiano na Masoko

### TBS MAKAO MAKUU

Shirika la Viwango Tanzania  
Barabara ya Sam Nujoma /  
Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam  
S. L. P. 9524  
DAR ES SALAAM, TANZANIA  
Simu Na: +255 22 245 0298/  
+255 22 245 0206  
Nukushi: +255 22 2450959  
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827  
Barua pepe: info@tbs.go.tz  
Tovuti: http://www.tbs.go.tz  
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya  
wateja: malalamiko@tbs.go.tz  
Twitter: TBS\_Tanzania  
Instagram: tbs\_Viwango

### TBS KANDA YA KATI

Jengo la Kambarage  
S. L. P. 2956  
DODOMA,  
TANZANIA  
Simu Na:  
+255 26 2520310

### TBS KANDAYA ZWA

Jengo la NSSF,  
Ghorofa ya 3  
S. L. P. 1814  
MWANZA,  
TANZANIA  
Simu Na:  
+255 28 2505044

### TBS KANDA YA KASKAZINI

Jengo la NSSF (Mafao  
House), Ghorofa ya 2  
S. L. P. 2399  
ARUSHA,  
TANZANIA  
Simu Na:  
+255 27 2520143

### TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI

Jengo la NHIF,  
Ghorofa ya 7  
S. L. P. 1674  
MBEYA, TANZANIA  
Simu Na:  
+255 25 2502848

### TBS KANDA YA KUSINI

Jengo la MTUWASA  
S. L. P. 1396  
MTWARA,  
TANZANIA  
Simu Na:  
+255 23 2334477

### TBS KANDA YA MAGHARIBI

Jengo la NSSF (Mafao  
House), Ghorofa ya 2  
S. L. P. 1276  
KIGOMA,  
TANZANIA  
Simu Na:  
+255 28 2804023

Barua zote ziandikwe kwa **MKURUGENZI MKUU**